



22110297



SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 1
SWAHILI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1
SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1

Wednesday 11 May 2011 (morning)
Mercredi 11 mai 2011 (matin)
Miércoles 11 de mayo de 2011 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire sur un seul des passages.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento.

Toa maoni yako juu ya **moja** ya tungo zifwatazo.

1.

Aliwaacha wanasheria wakate hukumu. Miaka na mikaka ilipita akitarajia. Akitarajia mtoto azaliwe, ampakate, ampe titi tamu la mama anyonye. Naye aambiwe na aitwe mama. Mama mzazi. Na kila uchao unakuja na kutarajia.

5 “Labda leo atazaliwa. Si walisema atazaliwa, na ni wangu? Kiu ya kungoja ni majaribio makubwa sana. Ah! Tamaa ya kutaka kuwa mzazi!”

Siku moja, madaktari na wakunga walikuja papa hapa wakamwambia wakati wakuzaa ulikuwa umewadia. Aliupokea kwa hamu na ghamu. Pupa na ari ya kupata mimba, kulea, kuzaa, ili kuleta kiumbe kipya duniani ilikuwa karibu impasue kifua.

10 Alihisi minofu ikiongezeka mwilini. Aliona mfuko wa mtoto ukipanuka ili kujiandaa kwa mgeni aliyekuwa akitarajiwa. Hata daktari na wakunga walisema maandalizi yalikuwa lazima. Walimwambia katika kuzaa, ilikuwa vyema kutahadhari kabla ya hatari. Ama, abebwaye hujikaza. Alielekeza juhudi zake zote kwa maandalizi.

Hakusita kwenda kwa wauza mboga na matunda kumshauri kuhusu lishe bora. Haya yote alifanya ili kusionua hisia zilizokuwa hazinjui kungoja au kutarajia.

15 Aidha alitembea akiimba kwa sababu ya kushiba furaha:

Nami niende

Langu lifutumue

Wasukume, nisukume

Nami talibwaga dume

20 *Nisimame nao kinyume*

Ama waunde tume.

Akikaanga *omena* au kambare aliimba kuwa ni sababu hakuwa mmoja, walikuwa jozi moja. Wawili. Hakuamini bahati yake. Wakati mwingine na kwa dakika nyingine, angebung'aa na kuuliza iwapo hata yeye angeweza kuitwa mzazi? Siku zingine akinunua mawe walayo akina mama, alisikia akimuuliza kwa kinywa kipana muuza mawe:

“Hata Nekesa? Hili tumbo linaweza kubeba? Siamini,” alimaliza.

Wanawake walicheka. Labda kutokana na tajriba na uzoefu wao wa kuzaa. Nekesa alikuwa mwana mkembe. Alipowaza kutafuta mafunzo, wajuwao walimwambia angoje pale pale mastakimu pake. Hakufanya kiherehere kupiga piga moyo.

30 Ni kweli alifika na mabuku. Walitoa na ya kuandika, kusoma, na mengine yenye picha kabambe Nekesa ayabandike ukutani. Mengi karibu na kalenda ili asikosee siku. Kumbe!

Wasemao husema, mambo kangaja huenda yakaja. Hakucheleva wala kucheleva kutoa dua na dakudura, mambo yasije yakakosa kumlainikia. Alitaka yawe shwari, au poa wasemavyo watu wa leo.

35 Alizinduliwa na daktari. Uzazi jamani?

“Mtoto utakaye mzaa ni wako. Je unajua? Si wetu. Ndio maana nimekuja kukupa elimu ili utoe malezi bora. Lakini sasa twataka maoni yako. Sisi tunatako uzae wa kiume. Hapana! Wa kike... La! Mzungu... au, muhindi ama... Ulitaka kumzaa mweusi au mweupe? Na..., ulitaka aabudu dini gani?”

40 Hakukumbuka kama alitoa maoni, au alijibu maswali. Alikuwa kashikilia tumbo lake tu.

Miaka na dahari, Nekesa bado anangonjea mtoto kuzaliwa. Mtoto wa Nekesa ni wake kweli? Kama kuzaa ni kwake, kwa nini aulizwe rangi? Kwa nini aulizwe dini? Kwa nini aulizwe jinsia?

45 Kwa sababu hakuwa na mtu wa kujibu, Nekesa alidhani ndivyo utaratibu wa kujifungua ulivyokuwa. Aliona lazima wanawake wote walipaswa kupitia hayo. Si hata yeye aliwahi kusikia bugudha za uzazi?

Hakuelewa maoni aliyoulizwa. Alifurahia kupewa fursa kuchangia tu. Hii ndiyo democrasia ya watu wanao fahamu uchungu wa uzazi. Ajuaye ni mama.

50 Mafunzo yenyewe alisikia yakiitwa; kiliniki, warsha, kongamano, na lugha nyingine ambayo kutokuwa na kisomo, “ijapo cha mama nipe kijiko,” hakuelewa alisikia tu wakiung’ng’a ati: sifolo edukesho.”

Maswali yake yalikuwa hata kujifungua mtoto wako, ilihitaji mikutano? Alitaka apewe ruhusa ya moja kwa moja awaambie kwa mhutasari sana kuwa, alitazamia mtoto tu. Hakuona kwa nini asumbuliwe.

55 Tena baada ya mafunzo, yaliyoandikwa kwa fotifoti, na kupelekwa huko mbali, kulikokuwa na taa nyingi, ambako usiku ulionekana kama mchana...

Owen McOnyango, *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (2006)

2.

Kuonana na Wewe

Kwamba risala afika, mjumbe wa ko'ngowea,
Angekuja na waraka mwema akakuletea,
Au ungalitamka maneno akakwambia,
Lakini hapana ndia ya kuonana na wewe.

5 Lakini hapana ndia ya muwanga ilo wazi,
Ndipo akalimatia kuja kwako matembezi,
P'enyenye ya kupenyeya siioni kwa maozi,
Ndipo hafanya ajazi ya kuonana na wewe.

10 Ndipo hafanya ajazi ningelikutokeleya,
Pasi kuona manyezi hatakasa yangu niya,
Ela nawacha walinzi walindao kulla mwiya,
Ndipo hujizuilia nisionane na wewe.

15 Ndipo hujizuilia, moyo unгатоaweza,
Kinyume haushikia, kisha nikauliwaza,
Nisiche kuukemea kwani utapata punguza,
Kwa kukosa mwangaza wa kuonana na wewe.

Kwa kukosa muwangaza muwanga unгazagaa,
Huona kikuu kiza nilipo nikiangaa.
Usambe vyanipendeza kwa hio sikukataa!
20 Napenda sikuliwaa la kuonana na wewe.

Napenda sikuliwaa, mwandani wangu mpenzi,
Kwa wema ulinitwaa kwa huruma na mbawazi.
Huwaje kukuwambaa, kwa leo, nyakati hizi?
T'afanyaje makatazi ya kuonana na wewe?

25 T'afanyaje makatazo kwako wewe mwana-ninga?
Ndiwe lulu ya mvazi, ipendezayo kutunga!
Ikapangua simanzi zamani za kujifunga.
Kukuata ni ujinga, kutoonana na wewe.

30 Kukuata ni ujinga ambao ni wa milele,
Nawe zidi kukitunga cheo chako si kitule;
Nakule kukibananga, ndiyo haya niketele,
Usambe linitukile la kuonana na wewe!

Usambe linitukile, mtanashati mrembo!
Mwana wa zilungu-pule, uso t’ua wala k’ombo!
35 Mambo wazi sitenzile, ukajandika misimbo!
Nalipenda lako umbo tuonanapo minawe!

MH Abdulaziz, *Muyaka* (1979)
